



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA

Unapojibu tafadhali taja
Kumb.Na. MDC/L.10/14/56

Tarehe: 27/04/2021.

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa ya kujaza nafasi moja (01) ya kazi ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja III**

1.0 NAFASI: MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III (NAFASI 01)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

- Mwenye elimu ya kidato cha nne (Form IV) au kidato cha Sita (Forma VI)
- Awe na Astashahada/Cheti NTA level 5 katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, maendeleo ya jamii, mipango na sayansi ya Siasa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

1.2 MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI III

Mwombaji atakayefaulu na kuajiriwa atatekeleza majukumu yafuatayo:

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao na kuwa Mlinzi wa Amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa mikutano/Vikao na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia sera, Kanuni, taratibu na Sheria za nchi
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali pamoja na kipato binafsi
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
- Mwenyekiti wa vikao vyote vya wataalamu katika Kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo ndogo za kijiji
- Atawajibika kwa mtendaji wa kata.

1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia muundo na ngazi za Mshahara ya watumishi wa serikali yaani **TGS/B/1** kwa mwezi

1.4 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- (a) Mwombaji awe ni raia wa Tanzania.
- (b) Awe na umri kuanzia miaka 18 na asiyezidi miaka 45.
- (c) Awe mtanzania mwenye akili timamu.
- (d) Maombi yote yaambatane na vivuli (photocopies) vya vyeti vya taaluma, ujuzi, cheti cha kuzaliwa, picha mbili (2) (Passport size) za rangi za hivi karibuni.
- (e) Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anuani na namaba za simu za kuaminika pamoja na majina matatu ya wadhamini (**Referees**) wa kuaminika.
- (f) Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**).
- (g) Maombi yandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
- (h) Waombaji wa kazi ambao tayari ni waajiriwa katika utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika waraka Na.CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30/11/2010.
- (i) Waombaji waliostaafu utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- (j) Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai.
- (k) "Testmonial" "Provisional Results" "Statement of Results" hati ya matokeo ya kidato cha nne au sita (Forma IV and Form VI Results Slips) HAVITAKUBALIWA.
- (l) Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- (m) **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10/05/2021 saa 9:30 Alasiri.**

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya wilaya ya Madaba,
S.L.P 10,
MADABA.**

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ambayo ni www.madabadc.go.tz pamoja na mbao za matangazo za Halmashauri.

Imetolewa na:


Shafi K. Mpenda
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA.**

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
MADABA DISTRICT COUNCIL
RUYUMA**